

TANGAZO LA USAJILI WA VIKUNDI VYA KIJAMII VYA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO INAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA VIKUNDI VYOTE VYA KIJAMII VYA KUWEKA NA KUKOPA KWA MAJINA YAKE (VICOBA, VSLA, HISA, LIMCA NK) VINATAKIWA KUSAJILIWA KWA MUJIBU WA SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA YA MWAKA 2018 NA KANUNI ZAKE ZA MWAKA 2019.


ILI KUSAJILI KIKUNDI UNATAKIWA KUFIKA OFISI YA AFISA MAENDELEO YA JAMII WA HALMASHAURI YA LUSHOTO UKIWA NA NYARAKA ZIFUATAZO:-

- i. FOMU YA MAOMBI YA USAJILI ILIYOSAINIWA NA VIONGOZI WA KIKUNDI- INAPATIKANI KWA AFISA MAENDELEO YA JAMII**
- ii. NAKALA 2 ZA KATIBA- WAWASILIANE NA AFISA MAENDELEO YA JAMII KWA KATIBA INAYOKIDHI VIGEZO**
- iii. NAKALA ZA MIHTASARI YA VIKAO VYOTE VYA UANZISHAJI WA VIKUNDI ILIYOSAINIWA NA WANACHAMA WOTE**
- iv. AZIMIO LA WANAKIKUNDI KUANZISHA KIKUNDI LILILOSAINIWA NA WANAKIKUNDI WOTE – FOMU YA AZIMIO INAPATIKANA OFISI YA AFISA MAENDELEO YA JAMII**
- v. ORODHA YA WANAKIKUNDI YENYE IDADI YA WANACHAMA WASIOPUNGUA 10 NA WASIOZIDI 50**

- vi. MUUNDO WA KIKUNDI
- vii. UTHIBITISHO WA MALIPO YA MICHANGO YA AWALI
- viii. BARUA YA UTAMBULISHO WA KIKUNDI KUTOKA KWA AFISA MTENDAJI WA KIJIKI/MTAA/KATA
- ix. JINA LA KIKUNDI LIWE LIMEJUMUISHA MANENO "KIKUNDI CHA KIJAMII CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA.....(ANDIKA JINA LA KIKUNDI MFANO UPENDO, FURAHA).

MWISHO WA USAJILI HUU NI TAREHE 30/04/2021. BAADA YA TAREHE HII KIKUNDI KITAKACHOFANYA SHUGHULI ZA KIFEDHA PASIPO KUSAJILIWA KITA KITATOZWA FINI YA FEDHA ZA KITANZANIA ISIYOPUNGUA MILIONI MOJA NA ISIYOZIDI MILIONI KUMI AU KIFUNGO KISICHOPUNGUA MIEZI 3 NA KISICHOZIDI MIAKA 2 AU VYOTE. USAJILI HUU HAUNA GHARAMA NI BURE.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA



IKUPA H. MWASYOGE
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
LUSHOTO

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
LUSHOTO